

# HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA



## TANGAZO LA KOTESHENI YA ULINZI WA HALMASHAURI YA JIJI.

1. Halmashauri ya Jiji la Arusha inakusudia kutumia huduma za kampuni watu Binafsi Ushirika Taasisi au Vikundi vya watu kwa ajili ya Ulinzi katika ofisi zake kipindi cha kuanzia **01.07.2018 hadi tarehe 30.06.2019**.
2. Halmashauri ya Jiji la Arusha inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, vyenye nia na uwezo wa kufanya kazi hii, kutuma maombi yao.
3. Mwombaji anaruhusiwa kuomba kotesheni zaidi ya mara moja kwa kadri ya uwezo wake.
4. Mwombaji wa kotesheni hii atalinda eneo la halmashauri ya jiji la Arusha kwa muda wote. 24hours
5. Kotesheni zote zitashughulikiwa kwa utaratibu wa ushindanishi wa waombaji wenyeji (Preferences to Local Community) kama ilivyoainishwa Kwenye Kanuni za Manunuzi (PPA 2011) –Kanuni ya 40 .GN 446 ya 2013 Kwa hiyo iko wazi kwa waombaji wenyeji wote wa jiji la Arusha.
6. Waombaji wote wenye nia na uwezo wanaweza kupata taarifa kamili kupitia makabrasha ya kotesheni katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni ya **Halmashauri ya Jiji la Arusha, barabara ya Boma S.L.P. 3013, Arusha**, kila siku kuanzia saa **2.30 asubuhi hadi saa 9:30 mchana**, siku za Jumatatu hadi Ijumaa chumba No.48 [kuondoa siku za sikukuu zinazotambulika kitaifa].
7. Nyaraka za kotesheni zinapatikana baada ya kulipa ada stahili ya kotesheni husika amabayo ni Tsh. 50,000/= (Elfu hamsini tu). Malipo ya maombi ya zabuni yafanyike kupitia akaunti ya Halmashauri ya Jiji la Arusha iliyoko katika Benki ya NMB, tawi la Clock Tower, akaunti ya Jumla Halmashauri ya **jiji Arusha. Account Na. 40801200336** na kuwasilisha nakala halisi ya hati ya malipo ya Banki [Bank Pay-in Slip, original copy] na kupata stakabadhi ya Halmashauri kwa zabuni iliyoombwa. Malipo yaliyotolewa Kama ada ya maombi ya zabuni hayatarejeshwa.

8. Kotesheni zote zifungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri [seal], na juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja aina ya kotesheni na namba ya kotesheni. Kotesheni hizo zipelekwe katika sanduku la zabuni lililoko katika ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji **chumba No. 66** kwa kutumia Anuani ifuatayo:-

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,  
Halmashauri ya Jiji,  
Barabara ya Boma,  
S.L.P. 3013, Arusha.**

Muda wa mwisho wakupokea maombi ya kotesheni ni **Tarehe 18.06.2018 siku ya Jumatatu saa 4:00 kamili asubuhi**. Maombi yote yatafunguliwa muda mfupi baadaye na kwamba waombaji wote au wawakilishi wao wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa kotesheni hizo.

9. Halmashauri ya Jiji la Arusha hailazimiki kukubali/kutokukubali kutoa kotesheni kwa mwombaji wa kotesheni yeyote kutokana na kigezo cha malipo makubwa/malipo kidogo ya eneo husika au utoaji huduma linaloombewa kotesheni.

**MKURUGENZI WA JIJI  
ARUSHA**